Baada ya kushuhudia hali ya mahali pale pamoja na upendo wa wale washirika kwa Mungu na furaha waliyokuwa nayo bila kujali mazingira yao, niliumia sana moyoni mwangu kiasi cha kutokwa machozi. ***Nilitafakari mambo mengi sana moyoni mwangu hasa jinsi ambavyo Mungu kwa neema yake amefanikisha mambo yangu binafsi lakini watu wake wanaomtafuta, wanamwabudu katika mazingira magumu kiasi kile tena bila kukata tamaa. Ghafla nikasikia kuguswa moyoni mwangu kwamba nitafute pesa katika vyanzo vyangu vya mapato ili nijenge kanisa mahali pale.***

Niliamini kuwa nitaweza kujenga bila msaada wa mtu mwingine kwa sababu nilikumbuka jinsi ambavyo Mungu alivyoniwezesha kwenye mambo yangu binafsi na tena mengine yalikuwa hayawezekani kabisa kwa akili za kibinadamu lakini kwa msaada wake yakawezekana.

***Hapo ndipo nilipata ujasiri kwamba je, Mungu atashindwa kunifanikisha jambo hili lililo jema mbele zake wakati mambo yangu anayafanikisha? Nikaamini bila shaka Mungu atanifanikisha***.

Wakati huo nilikumbuka kisa cha mtumishi wa Mungu ***Nehemia*** jinsi alivyoguswa na hali ya kuharibika kwa ukuta wa Yerusalemu na alipoazimia moyoni mwake kuujenga, Mungu alimfanikisha. Hivyo nikaamini kwamba, kwa kuwa Mungu wa Nehemia anaishi hata sasa, atatenda kwangu pia.

Kabla ya kujua ni jinsi gani nitapata fedha za ujenzi, niliazimia kufunga na kuomba kwa muda wa siku **saba (7)** ili Mungu aseme na mimi jinsi ya kupata fedha na pia kunipa kibali mbele zake kwa ajili ya kazi hiyo. Wakati ninaendelea na maombi, nikiwa ofisini kwangu, nilitembelewa na mtumishi wa Mungu aitwaye **Leonard Joseph**. Wakati tukiongelea masuala mbalimbali ya huduma ya Mungu, nikamwonesha picha za mahali pale nilipotembelea. Alipoziona, pia aliguswa sana, nikamwambia nina mpango wa kujenga Kanisa mahali hapo na yeye akaniahidi kuwa nitakapokuwa tayari kuanza ujenzi nimshirikishe naye atachangia.

Aliponiambia kuhusu kuchangia kazi ya ujenzi, ghafla nikasikia moyoni kufunuliwa na kuoneshwa kwamba badala ya kufikiria kuwa naweza kujenga peke yangu kwa fedha zangu, kumbe naweza kushirikisha baadhi ya watu wenye nia ya kuchangia na hatimaye tukajenga kwa pamoja. *Lakini pamoja na hivyo, niliazimia moyoni mwangu kuwa sitamshirikisha mtu yeyote ninayemwona kwa akili na macho yangu hata kama najua yupo na pesa nyingi bali nitaendelea na maombi na Mungu mwenyewe atanionesha ni nani nimshirikishe katika kuchangia*. Ninamshukuru Mungu kwa uaminifu wake maana ni kweli alianza kunionesha watu wa kushirikisha na ili kuthibitisha hilo kila niliyemshirikisha alipokea kwa furaha sana na hakuna aliyeahidi kuchangia chini ya shillingi **milioni moja,** fedha za kitanzania. Kiasi hicho cha fedha hakikuwa kidogo kwa wakati huo na hasa